

Vermont health information exchange



Hii ni nini?

Kwa hivyo Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont ni nini?

Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont kinaweka rekodi zako za afya katika hifadhi salama. Unapomuona daktari ama mhadumu wa kiafya anayeshiriki, ujumbe wa rekodi ya kielektroniki unaweza kutumwa kwa Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya. Rekodi hii iko tayari kwa daktari utakayekutana naye muda mfupi ujao kwa hivyo, wanajua historia yako ya kiafya. Daktari huyu anaongezea taarifa hizo kwenye rekodi zako ili iwe tayari kwa daktari anayefuata, kwa usanjari huo.

Inamfanya mtoa huduma wako kujua kila kitu kinachoendelea kukuhusu.



Machaguo yangu ni yapi?

Kwa kuwa sasa unajua mambo mengi kuhusu Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont, wacha tuzungumze kuhusu machaguo yako.

Shiriki

Iwapo unataka manufaa ya watoa huduma wako wote walio na rekodi zako za kiafya basi huna jinginelolote la kufanya. Iwapo watoa huduma wako watashiriki, rekodi zako zitasambazwa kwenye Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya.

Pata taarifa zaidi kabla ya kufanya maamuzi

Daktari ama mtoa huduma wako wa afya anaweza kujibu maswali kuhusu Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya. Ama unaweza kupiga simu katika Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya kupitia kwa **1-888-980-1243**.

Usishiriki

Unaweza kuchagua kutokubali rekodi zako za kifaya kusambazwa kwa watoaji huduma za kiafya. Hatua hii inaitwa kujiondoa kwa hiari. Ikiwa utajiondoa, rekodi zako zitahifadhiwa kwenye Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya. Lakini watoaji huduma wako hawataweza kuziona rekodi hizo, isipokuwa katika hali za dharura.

Ili kujiondoa, tembelea **VTHealthInfo.com** ili kukamilisha ama kupakua fomu ya kujiondoa au piga simu kwa Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya kupitia kwa Simu ya moja kwa moja ya **1-888-980-1243**.

Iwapo una maswali na unataka kuzungumza na mhadumu binafsi ambaye hahusiani kabisa na Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont, piga simu ya moja kwa moja ya Wakili wa Huduma ya Afya kupitia 1-800-917-7787.



VTHealthInfo.com

Kwa maswali zaidi, piga simu ya moja kwa moja kwa Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya kupitia 1-888-980-1243.

Vermont health information exchange



Kuna nini kwenye rekodi yangu?

Rekodi za mgonjwa zinaweza kuhusisha:

- Demografia ya mgonjwa (kama vile jina, umri, tarehe ya kuzaliwa, anwani)
- Magonjwa
- Majeraha
- Hali
- Mizio
- Matibabu
- Matokeo ya vipimo vya maabara
- Ripoti za kirediolojia
- Taarifa fupi za huduma ya mgonjwa
- Maelezo ya Daktari
- Taarifa finyu ya afya ya kiakili*
- Taarifa finyu kuhusu kasoro inayosababishwa na matumizi mabaya ya dawa* (pia huitwa uraibu)

* Rekodi kuhusu matibabu ya afya ya kiakili pamoja na kasoro inayosababishwa na matumizi mabaya ya dawa yaliyotolewa katika huduma za kimsingi, idara za dharura, pamoja na hospitali zinaweza kushirikishwa. Rekodi hizi zinaweza kuhusisha uchunguzi wa vipimo pamoja na maelekezo ya kimatibabu. Kwa wakati huu, wataalamu wa kibinafsi wa mgonjwa ya akili, washauri nasaha wa afya ya akili pamoja na vituo vya matibabu ya kasoro zinazosababishwa na utumiaji vibaya wa dawa havichangii kwenye Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont.

Kwa taarifa zaidi, tembelea VTHealthInfo.com/FAQS

Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya cha Vermont kinaendeshwa na Viongozi wa Teknolojia ya Habari wa Vermont (VITL) na kadhalika kinafadhiliwa na Jimbo la Vermont kama huduma kwa wenyeji wote wa Vermont. Kwa taarifa zaidi kuhusu VITL, tembelea VITL.net



Inamaanisha nini kwangu?

Ikiwa mnaelewana vyema baina yako na madaktari pamoja na watoaji wako wa huduma za kiafya huwa ni njia mojawapo rahisi ya wewe kupata huduma bora za kiafya.

Watoaji huduma wanapotumia Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya, huwa wanafikia rekodi hizo za pamoja. Hii inamaanisha kwamba hutahitajika kujibu swali lilo hilo kila mahali. Ama ukumbuke mambo yalipotokea. Ama ujue kwa uhakika ni dawa zipi ulizotumia. Na iwapo hutoweza kabisa kutoa taarifa, kama unapokuwa kwenye hali ya dharura, bado Daktari anaweza kupata taarifa muhimu ili kukusaidia.



VTHealthInfo.com

Kwa maswali zaidi, piga simu ya moja kwa moja kwa Kituo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Kiafya kupitia 1-888-980-1243.